Jehanamu Ni Halisi

(Hell Is Real)

Na

Ellis P. Forsman

Jehanamu Ni Halisi

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 12, 2011

Jehanamu Ni Halisi

Ufu. 1:18

Ufu. 1:18, "*Na aliye hai; nami nalikuwa nimekufa, na tazama ni hai hata milele na milele. Na ninazo funguo za mauti na za kuzimu.*"

Wazo la adhabu ya milele limeandikwa na watu wengi kama moja ya kumbukumbu hizo kutoka katika ushirikina wa zamani. Kilichotawala leo ni kuhusu injili ya kijamii, na mwanga wake, dhaifu, hotuba kuhusu amani, kujitolea, wema, udugu, na sinazofanana na hizo, na makanisa ambayo hayasikii somo la jehanamu likitajwa.

Na kejeli yake ni kweli kwamba watu wengi ulimwenguni leo wako njiani kuelekea jehanamu, alafu ni moja ya somo la mwisho linalotajwa kwenye Biblia.

Mat. 7: 13-14, "*Ingieni kwa kupitia mlango uli mwembamba, maana mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. Bali mlango ni mwembamba, na njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache.*"

Biblia inayotuambia uzuri wa mbinguni pia inatuambiaa kuhusu jehanaamu ilivyo mbaya. Mungu anatuambia kwamba kuna jehaanamu ya milele kwa wale wote wanaomkataa Kristo na injili yake.

2 Thes. 1:7-9, "*Na kuwalipa ninyi mteswao raha pamoja na sisi; wakati wa kufunuliwa kwake Bwana Yesu kutoka mbinguni pamoja na malaika wa uweza wake katika mwali wa moto; huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii injili ya Bwana wetu Yesu; watakaoadhibiwa kwa maangamizi ya milele, na kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake;*"

Wengi ni wanadamu walionena kwa uasi neno la Mungu, wakikataa uwepo halisi wa jehanamu, au kwamba mwanadamu ana nafsi.

Mwanadamu ana nafsi

Waalimu wa uongo wana muda na tena wamemkataa Mungu, kazi ya Mungu, Kristo, na Roho Mtakatifu katika uumbaji, na hata kukataa kwamba mwanadamu ana nafsi pamoja na makazi ya milele.

Watu kama Charles T, Russell and Judge Rutherford, mababu wa mashahidi wa Yehova, wanakataa kwamba mwanadamu ana nafsi. Rutherford alisema, "Hayupo mwanadamu aliye na nafsi! … Wahubiri wamewafanya watu waamini kwamba mwanadamu anabeba nafsi ndani yake na kwamba akifa nafsi itachomoka naa kwenda sehemu nyingine. … Kifo ni wakati kamili wa kutokuwepo."

Ni tofauti kiasi gani kutoka katika ukweli wa Mungu!

Fikiria kwamba mtu wa dini anatoa kauli kama hiyo? Bila kujali kwamba kuna imani nyingi duniani.

Yesu alisema katika Yohana 5:28-29, "*Basi Yesu akapaza sauti yake hekaluni akifundisha na kusema, mimi mnanijua na huko nitokako mnakujua; wala sikuja kwa nafsi yangu; ila yeye aliyenipeleka ni wa kweli, msiyemjua ninyi. Mimi namjua kwa kuwa nimetoka kwake, naye ndiye aliyenituma.*"

Lazima izingatiwe kwamba Yesu alisema, "*...wote wwalioko makaburini watasikia sauti yake na watamwendea...*" wote "*wema*" na "*waovu*" siyo tu waliokolewa. Watu wengine wanaamini kwamba watu waovu wakifa wanakwenda moja kwa moja jehanamu. Sivyo.

- Mdo. 24: 15, "*... kutaakuwa na ufufuo wa wafu, wenye haki na wasio haki pia.*"
- 1 Thes. 4:16-17, "*Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele. Basi farijianeni kwa maneno hayo.*"
- 1 Pet. 4: 17-18, "*Kwa maana wakati umefika wa hukumu kuanzaa katika nyumba ya Mungu; na ikianza kwetu sisi mwisho wao wasioitii injili ya Mungu utakuwaje? Na mwenye haki akiokoka kwa shida, yule asiyemcha Mungu na mwenye dhambi ataonekana wapi.*"

Hukumu haitaanza mpaka Kristo arudi. Mhu. 12:7, "*Nayo mavumbi kuirudia nchi kama yalivyokuwa, nayo roho kumrudia Mungu aliyeitoa.*"

Nafsi ya mwanadamu haifi.

Jehanamu ni elimu ya Biblia

Lazima tuhubiri kuhusu jehanamu kwa sababu ya mafundisho ya neno la Mungu. Mtu wa Mungu ana wajibu ya kuwaonya watu kuikimbia ghadhabu ya Mungu. Tunahitaji kuwaambia watu kuhusu jehanamu, na kuwa na machozi kwa wale waliopotea. Tunapaswa kuwaambia waliopotea kuhusu Mwokozi wetu aliyekufa ili kuwaokoa kutoka jehanamu!

Ni lazima tuhubiri kuhusu jehanamu ili kuwaonya wenye dhambi! Rafiki zangu, je umewahi kuzingatia ukweli kwamba utakuwa jehanamu kwa dakika ijayo?

Daudi wa wakati wa Agano la Kale alisema katika 1 Sam. 20:3, "*...iko hatua moja tu kati ya mimi na mauti.*"

Wapendwa, ni hatua tu kufika umilele!ndiyo, lazima tuhubiri kuhusu jehanamu kwa sababu watu wanakufa kila siku bila Kristo. Kwa bahati mbaya kila mtu anayo dakika moja pekee – dakika moja imebaki kabla ya mwisho wake, makao ya milele, mbinguni au jehanamu! Je umewahi kufikiria kuhusu umuhimu wa ahadi hii kuu?

Wanawake na wanaume, **kuna** sehemu ya adhabu ya milele iitwayo jehanamu! Imetunzwa kwa ajili ya shetani na malaika wake, na kwa wale wanaomfuata Shetani, waliomkataa Kristo. Mungu alisema hivyo, Kristo akasema hivyo, mitume na waandishi waliovuviwa pia walisema hivyo.

Hakuna jehanamu, dhambi nyingi

Jibu dhahiri katika umri wetu ni kwamba tuna dhambi isiyo dhibitiwa katika jamii yetu!

Motto anapotambua kwamba kutakuwa na adhabu anapokosa utii kwa wazazi wake, anapaswa kujifunza utii kwa mamlaka sahihi nyumbani, na mara katika maisha yote ya mahusiano.

Kwa upande mwingine, huyo mtoto akitambua kwamba hakutakuwa na adhabu yaa kutotii kwake ataendelea katika njia zote za kutotii na uasi.

Katika jamii, kama wanadamu wanadhani wanaweza kuua na kuiba bila kupewa adhabu ya uhakika, ni vigumu kwao kusita wanapojaribiwwa kufanya hivyo.

Wengi wanadhani kwamba wana maisha haya tu na wanapokufa hakuna kinachobaki.

Vivyo hivyo kwa kutii neno la Mungu, kama mwanadamu anadhani anaweza kuishi maisha ya dhambi na hata adhibiwa milele, kwa vyovyote atakuwa na ukomo.

Heb. 10:26-31, "*Maana kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi; bali kuna kuitazamia hukumu yenye kutisha, na ukali wa moto ulio tayari kuwala wapingao. Mtu aliyeidharau sheria ya Musa hufa pasipo huruma kwa neno la mashahidi wawili au watatu. Mwaonaje? Haikumpasa adhabu iliyo kubwa zaidi mtu yule aliyemkanyaga Mwana wa Mungu, na kuihesabu damu ya agano iliyotakaswa kwayo kuwa ni kitu ovyo na kumfanyia jeuri Roho wa neema. Maana twamjua yeye aliyesema, kupatiliza kisasi ni juu yangu mimi nitalipa. Na tena Bwana atawahukumu watu wake. Ni jambo la kutisha kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai.*"

Ndiyo, wanadamu wamesahau ghadhabu naa haki ya Mungu Mkuu.

Ufu. 20: 12-15, "*Nikawaona wafu wakubwa kwa wadogo wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi; na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao. Bahari ikawatoa wafu waliokuwemo ndani yake na mauti na kuzimu zikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake. Wakahukumiwa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake.*"

Ni nani anayeamini katika Jehanamu?

Mara kumi na moja Yesu alitumia neno la Kiyunani Gehenna kuelezea jehanamu.

Katika Marko 9:48, "*...humo funza wao hafi, wala moto hauzimiki.*"

Mwana wa Mungu alifahamu yote kuhusu jehanamu, na akanena waziwazi na kwa ujasiri kuhusu mambo kama hukumu, moto, kuangamia, na mateso. Yesu alisema mambo haya kwa sababu anatupenda na hataki tupotee jehanamu.

2 Pet. 3:9, "*Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee bali wote wote wafikilie toba.*"

Mtu Paulo aliandika kuhusu ufunuo wa Bwana kutoka mbinguni: 2 Thes. 1:8-9, "*Katika mwali wa moto huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu.*" *Yesu;watakaoangamizwa kwa maangamizi ya milele, kutengwa na uso wa Bwana na utukufu wa nguvu zake;*

Hata hivyo Paulo alikuwa muhubiri mwenye nguvu wa rehema za Mungu na wokovu wa mwanadamu kwa imani inayotii; alafu pia alijua kuwa mshahara wa dhambi ni mauti!

Vilevile, mtume Yohana (mtume wa upendo, kama alivyoitwa) aliamini katika Jehanamu.

Kitaabu cha Ufunuo wa Yohana, kilichoandikwa na Yohana, kinatoa taswira siyo tu uzuri na furaha ya mbingu, lakini pia sehemu inayoitwa jehanamu. Sikiliza maneno ya Yohana alipoandika kwa uvuvio: Ufu. 21:8, "*Bali waoga na wasioamini, na wachukizao,, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili.*"

Jehanamu ni halisi!

Kuzimu **Tartar**

"Paradiso"

Hukumu

Ge- Hinnon (Kiyu **Mbinguni**

Jehanamu

Mabibi na mabwana, ulimwengu wa dini hausikii mengi kuhusu jehanamu kutoka kwenye mimbari yao ya kisasa, au siyo?

Mungu ametangaza,

- Rum. 3:23, "*Kwa sababu wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu.*"
- Rum. 6:23, "*Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.*"

Jehanamu, kuzimu, paradise, tartar.

Kuna maneno matatu ya Kiyunani, kila moja inaelezea sehemu tofauti, ambayo inaajumuishwa kaatika neno moja laa "jehanamu" katika Biblia ya toleo la Mfalme Yakobo. Ukweli huu umesababisha mkanganyiko mkubwa miongoni mwa waatu wengi katika uelewa wao, au kutokuelewa Biblia kuhusu somo hili.

Neno la Kiyunani, "Kuzimu" (ambalo ni sawa na neno la Kiebrania, "Kuzimu") ni "isiyoonekanaa" au "inayopokea yote" sehemu ambapo nafsi za wafu zinakwenda kusubiri hukumu.

Hapa nddipo Yesu alienda alipokufa msalabani.

Katika Mdo. 2:31, Petro ananukuu Zab. 16:10, "*Maana hutakuachia kuzimu nafsi yangu, wala* **(Kuzimu)** *hutamtoa mtakatifu wako aone uharibifu.*"

Yesu hakwenda katika sehemu ya mateso, maana hiyo ilikuwa haijafika. Alikwenda katika sehemu ya kusubiria, ambayo alipaita "Paradiso."

Luka 23:39-43, "*Na mmoja wa wale wahalifu waliotungikwa alimtukana akisema, Je! Wewe si Kristo? Jiokoe nafsi yako na sisi. Lakini yule wa pili akamjibu, akamkemea, akisema, wewe humwogopi hata Mungu, nawe u katika hukumu iyo hiyo? Nayo ni haki kwetu sisi kwa kuwa tunapokea malipo tuliyostahili kwa matendo yetu; bali huyu hakutenda lo lote lisilofaa. Kasha akasema, Ee Yesu, nikumbuke utakapoingia katika ufalme wako. Yesu akamwambia, amin, nakuambia leo hivi utakuwa pamoja name peponi.*"

Kumekuwa na mikanganyiko mingi kuhusiana na kifungu hiki. Ulimwengu wa dini wanadai kwamba mwizi msalabani aliokolewa. Alimuomba Yesu amkumbuk, akidhani kwamba watakwenda uelekeo tofauti baada ya kifo chao. Yesu alisema watakuwa pamoja tena baada ya masaa kadhaa katika sehemu aliyoiita Paradiso, ambayo pia ilikuwa Kuzimu, sehemu ya kusubiria. Kama mwizi aliokolewa, haikuwa kama Mkristo, maana bado alikuwa anatokana na uzao wa Kiyahudi.

Pia, tufahamu ya kuwa Yesu alikuwa bado hajapaa kwenda katika paradise ya mbinguni, maana baada ya ufufuo wake alimwambia Mariamu Magdalena aliyekuwa amesimama nje ya kaburi akilia: "*...Usinishike kwa maana <u>sijapaa</u> kwenda kwa Baba. Lakini enenda kwa ndugu zangu ukawaambie, ninapaa kwenda kwa Baba yenu, kwa Mungu wangu naye ni Mungu wenu.*" (Yohana 20:17).

Hii inaongelewa katika wakati ujao.

Tumeongelea “Gehena,” ambayo ni sehemu ya mateso ya milele iliyotunzwa baada ya hukumu, lakini ningependa kusema mambo machache kuihusu.

Hiki ni Kiyunani kiwakilishi cha Kiebrania “Ge-Hinnon,” ambayo ilikuwa ndefu, shimo pana kusini mwa Yerusalemu, ambapo Wayahudi waaabudu sanamu waliwatoa sadaka watoto wao kwa mungu Moleki. Baada ya wakati wa Yosia, tendo hili lilikoma, na sehemu hii ikawa sehemu maarufu ya kutupwa uchafu ya Yerusalemu, ambapo kila aina ya uchafu, mizoga, na miili ya wahalifu ilitupwa. Kulikuwa na mwendelezo wa moto na moshi ukipanda kutoka bondeni, na ikawa ishara ya sehemu yenye mateso yasiyokoma kwa waovu.

Hata hivyo kuzimu kutatupwa katika ziwa la moto pia. Ufu. 20:14, “*Mauti na kuzimu zitatupwa katika lile ziwa la moto. Hii ndiyo mauti ya pili, yaani hilo ziwa la moto.*”

Kama kulikuwa na aina moja ya jehanamu tu, isingeleta maana kusema kwamba jehanamu ilitupwa katika jehanamu.

Kuna neno linguine la Kiyunani iliyotafsiriwa kama “jehanamu” – ambayo ni “Shimo”.

Hili neno linatumika mara moja tu katika maandiko. 2 Pet. 2:4, “*Kwa maana ikiwa Mungu hakuwaachilia malaika waliokosa, bali aliwatupa shimoni, akawatia katika vifungo vya giza, walindwe hata ije hukumu;*”

Hii siyo Kuzimu au Gehena.

Hii ni sehemu iliyoandaliwa kwa ajili ya malaika waliotenda dhambi na pia walikuwa wanasubiri hukumu. Wamefungwa, au wamezuiwa pale.

Nafsi zote zimetunzwa katika kuzimu

Watu wote ni lazima wafe, ahadi ambayo dhahiri, na baada ya kifo, hukumu. Heb. 9:27, “*Na kama vile watu wanavyowekewa kufa mara moja, na baada ya kufaa hukumu.*”

Hataivyo, nafsi ya mwanadamu anapokufa, haziendi moja kwa moja kuhukumiwa mbele za Mungu alafu badae mbinguni au motoni (Jehanamu), kama inavyodhaniwa na watu wengi.

2 Kor. 5:10, “*Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele za kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara mambo aliyotendaa kwa mwili, kaadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya*.”

Hukumu ni kwa wakati mmoja inatatokea baada ya Yesu Kristo kurudi tena ulimwenguni hapa, ambapo kwa wakati huu sote tutakusanywa pamoja mbele za Bwana Mungu.

Mwanadamu anapokufa, nafsi yake huendaa kuzimu kusubiri hukumu. Baada ya hukumu, waovu na wasioamini watatupwa katika ziwa la moto kwa ajili ya adhabu ya milele.

1 Thes. 4:14-18, “*Maana ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa aakafufuka, vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye. Kwa kuwa twawaambieni haya kwa neno la Bwana kwamba sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana, hakika hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti. Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa*

katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kasha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele. Basi farijianeni kwa maneno hayo."

Kuelewa ambacho mtume Paulo alisema: Yesu akirudi tena wafu wafao katika Kristo watafufuliwa kumpokea Bwana mawinguni, alafu wale walioko hai ndani ya Kristo pia watakwenda kumpokea Bwana. Kabla ya hukumu kuja.

Wengine wanadhaani kwamba wakifa siku ya hukumu ni kwa wakati huo kwao na mara wanakwendaa mbinguni au motoni. Sivyo! Hukumu ni wakati aambapo wote watasimama mbele za Bwana kwa wakati mmoja. Na wakati huo bado mpaka Yessu atakaporudi kutoka mbinguni kwa sauti kuu na sauti za tarumbeta ya Mungu ambayo kila mmoja ataweza kusikia.

Wakati huo wa mwisho hautakosewa.

Kumekuwa na nyakati katika historia yetu ambapo watu fulani wa dini wamedai kwamba Bwana amerudi kisirisiri kwao kama vile Mashahidi wa Yehova mnamo 1918.

Hakutakuwa na muonekano wa kisiri wa Bwana. Atakaporudi tena, kila mmoja atafahamu.

Hakuna ahadi ya yeyote kwenda katika sehemu ya mwisho, iwe mbinguni au motoni, mpaka baada ya hukumu.

Wengine pia hudhani kwamba wale ambao siyo viungo vya Kristo watakwenda moja kwa moja motoni; kwamba hukumu hiyo itakuwa tu kwa ajili ya washirika wa Kristo. Sivyo.

Maandiko yanasema kwamba Mungu atawahukumu watoto wake, alafu awahukumu wengine pia. 1 Pet. 4:17-18, "*Kwa maana wakati umefika wa hukumu* ***kuanza*** *katika nyumba ya Mungu; na ikianza kwetu sisi, mwisho wao wasioitii injili ya Mungu utakuwaje? Na mwenye haki akiokoka kwa shida, yule asiyemcha Mungu na mwenye dhambi ataonekana wapi?*"

Kwa wale ambao hawajawahi kufanyika Wakristo kwa njia ambayo Mungu ameionyesha, hukumu ya Mungu kwao inaweza ikawa fupi sana.

Mat. 7:21-23, "*Si kila mtu aniambiaye Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni. Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jinaa lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu*."

Wale anaofahamu kwamba majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima chaa Mwana-kondoo, kama wale amabo Petro aliandika. Fil. 4:3, "*Naam, nataka na wewe pia mjoli wa kweli, uwasaidie wanawake hao kwa maana waliishindania injili pamoja name, na Klementi naye na wale wengine waliotenda kazi pamoja name, ambao majina yao yamo katika kitabu cha uzima.*"

Hata ivyo, haitakuwa vizuri kwa wale wasio na majina yako katika kitabu cha uzima cha mwanakondoo. Ufu. 20:15, "*Na upanga mkali kutoka kinywani mwake ili awapige mataifa kwa huo. Naye atawachunga kwa finbo ya chuma, naye anakanyaga shinikizo la mvinyo ya ghadhabu ya Mungu Mwenyezi.*"

Ndani ya hicho kitabu yameandikwa maisha yote ya Mkristo, yote mema na mabaya. Ufu. 20:12, "*Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimaama mbele ya hicho kiti cha enzi; na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa ambacho ni chaa uzimaa; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao.*"

Tunapaswa kuhubiri teno. Lakini pia kuna onyo kwetu kwamba tukishindwa kuliteteaa neno la Mungu, majina yetu yatafutwa.

Ufu. 22:19, "*Na mtu yo yote aakiondoa lolote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima, na katika ule mji mtakatifu ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki.*"

Sidhani kama kuna mmoja wetu atakaayependa kukutana na ghadhabu ya Mungu kama majina yetu yameandikwa na kufutwa kwa sababu yoyote, tuwe tumemkataa au kutolitunzaa neno lake.

Hataivyo, tukiwa waaminifu kwake, hatafuta majina yetu katika kitabu chake cha uzima. Ufu. 3:5, "*Yeye ashindaye atavikwa hivyo mavazi meupe, wala sitalifuta kwamwe jina lake katika kitabu cha uzima, name nitalikiri jina lake mbele za Baba yangu, na mbele ya malaika zake.*"

Ziwa liwakalo moto na kiberiti

Mara nyingi swali linaulizwa, "Kwa vile Biblia inaongelea moto mara nyingi, je jehanamu ni sehemu yenye moto halisi?"

Hatujui kwamba itakuwa ni moto halisi, lakini tunajua kwamba itakuwa ni maangamizi mabaya ya milele, kana kwamba kuvumilia moto usiozimika.

Kunaweza kusiwe na mateso yaliyosemwa katika akili ya mwanadamu kama ule wa moto wa milele. Hata moto halisi tunaoufaahamu leo inaumiza na haivumiliki. Tunaweza kupata maumivu makuu na mateso zaidi kuliko ile ya moto.

Ufu. 21:8, "*Bali waoga na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndio mauti yaa pili.*"

Rafiki wapendwa, huwezi tu kwenda jehanamu!

Jehanamu si mzaha

Wapendwa, jehanamu si utani! Inaweza ikawa kwenye nafasi ya juu kwenye sehemu ya utani; inaweza kuonekana kwenye vazi jekundu la ibili la ndani, ikiwa na pembe na mkia. Mzaha unaweza kujumuisha agizo la shetani la kuzoa mkaa haraka, na aina nyingi za rangi zinazofanana na kuweza kusisimua wacheshi walioko kwenye umati.

Lakini nawaambia jehanamu hakuna mzaha! Jehanamu ni ukweli unaotisha!

Heb. 10:31, "*Ni kitu cha kuogofya kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai.*"

Jehanamu – Milele pamoja na waovu

Marafiki zangu, watu wengi huuliza swali hili, “Jehanamu inafananaje?”

Sawa, neno la Mungu linasema wazi kwamba moja ya sifa ya jehanamu ni mateso ya milele ikishirikisha waovu wa karne zote.

Jehanamu ni sehemu ambayo nafsi iliyopotea lazima iende pamoja na wenye dhaambi waliokithiri ambao hawajawahi kuishi, pamoja na Shetani na mapepo yake yote.

Ndiyo, wauwaji na wahalifu, na wengine wote wa aina kama hao, pamoja na makahaba, walevi, wasioamini kwamba Mungu yupo, waabudu sanamu, waongo, wazinzi, na jamii yote iliyopotea watakuwa katika jehanamu ya milele; na acha niwaambie hili, kama tunapaswa kwenda pale, tutakuwa katikati yao milele!

Je unataka kutumia umilele na Shetani mwenyewe?

Ufu. 20:10, “*Na yule ibilisi, mwenye kuwadanganya, akatupwa katika ziwa la moto na kiberiti alimo yule mnyama na nabii wa uongo. Nao watateswa mchana na usiku hata milele na milele.*”

Ndiyo, tukipotea jehanamu tutasugua mabega pamoja na waovu na wabaya zaidi, watu wenye tama na waovu. Ukifa kama hujaokolewa, unapaswa kwenda katika takataka ya jehanamu milele – motoni!

Jehanamu – kutengwa milele

Rafiki zangu, wakati fulani Yesu aliwaambia viongozi wa dini ambao walikuwa hawajaokolewa kuhusu wakati wake:

Luka 13:28, “*Ndipo kutapokuwa na kilio na kusaga meno, mtakapomwona Ibrahimu na Isaka na Yakobo na manabii wote katika ufalme wa Mungu, nanyi wenyewe mmetupwa nje.*”

Itakuwa ni mshituko wa aina gani kwao.

Kwa Wayahudi, milele ingekuwaa karne nzuri kama wangekuwa na mababa wa taifa lao. Jinsi walivyotamani kuwa na Ibrahimu, Isaka, Yakobo, Musa, Danieli, Daudi, na manabii wote wakubwa wa Agano la Kale!

Yesu aliwaambia Wayahudi hawa kwamba kulia na kuomboleza itakuwa wakati watakapo gundua kwamba hawatakuwa pamoja na wale waliowaheshimu zaidi.

Wengi wetu tunafikiria mbingu kwa mtazamo wa muunganiko na mpendwa wetu aliyetangulia, kama vile mama wa Mkristo, baba wa kimungu, mume, au mke, au labda motto aliyenyakuliwa akiwa mchanga.

Tunafikiria mbingu kwa mlengo wa sehemu ya ushirika pamoja na Mwokozi aliyetufia msalabani.

Tunatamani kuona na kuongea na Petro na Paulo, Yakobo, na Yohana, na majeshi yote ya Wakristo toka zamani hadi sasa.

Itakuwa ni mateso mabaya kiasi gani kwa yeyote kati yetu tukitenganishwa milele na wapendwa wetu na marafiki!

Katika jehanamu hayupo atakayefurahia ushirika au urafiki.

Ukipotelea jehanamu, na wapendwa wako wote na marafiki wako pale, hutakuwa na urafiki wenye upendo, hakuna ushirika mtamu pale.

Jehanamu ni sehemu yenye giza lilokamilika, pamoja na kilio na maombolezo, na kusaga meno.

- Hakutakuwa na nyakati nzuri, hakuna sherehe jehanamu!
- Itakuwa ni sehemu ya huzuni ya milele!
- Hakutakuwa na wakati wa furaha na kicheko.
- Hayupo anayeweza kufurahi kwenye mateso, maumivu, huzuni, pamoja na kulia, kuomboleza, na kusaga meno ya kila upande!
- Lakini mbaya kuliko vyote, itakuwa ni utengano kamili na Mungu.

Giza la Milele

Mabibi na mabwana, jehanamu ni nini? Moja ya kitu kinachotisha ya uhalisia wa jehanamu ni ile ya giza la milele.

Yuda 1:13, "*Ni mawimbi ya bahari yasiyozuilika, yakitoa aibu yao wenyewe kama povu; ni nyota zipoteazo ambao weusi wa giza ndio akiba yao waliowekewa milele.*"

Unaweza kuanza kufikiria kuwa katika sehemu kama hiyo? Sehemu ambayo mionzi ya jua haijawahi kuwaka, ambapo utukufu wa nyota na mwanga wa mwezi havionekani, haipenyezi giza dhabiti usiku wa milele.

Ebu fikiria sehemu ambayo haina mchana – usiku upo milele?!

Kama unaweza kutazama weusi huu wa milele, unaweza kutambua moja – moja pekee – ya mateso ya jehanamu.

Ndugu, je mnawazo lolote la milele ina muda gani?

Historia ya mwanadamu duniani ni karibia miaka 6000.

Kipindi cha mababu ulianza karibia miaka 4000 kabla ya Kristo.

Ahadi ya Mungu kwa Ibrahimu ilikuwa karibia miaka 2000 kabla ya Kristo.

Siku ya Pentekoste (kanisa lilipoanzishwa) ilikuwa miaka 30 baada ya Kristo.

Na wakati wa Wakristo sasa una umri wa miaka 1981 (wakati 2011).

Yote kwa yote, historia ya mwanadamu ni karibia miaka 6000.

Kumbuka Ayubu alisema kwamba baada ya maisha haya siku zake zitaongezeka kama mchanga.

- Ayubu 29:18, "*Ndipo niliposema nitakufa ndani ya kioto change, nami nitaziongeza siku zangu kama mchanga;*"
- Zaburi 90:10, "*Siku za miaka yetu ni miaka sabini.*"

Mifungo mitatu na kumi ni miaka 70; mifungo mine ni miaka 80. Wengine wanaishi kidogo; wachache wanaishi miaka 100.

Tuseme punje moja la mchanga inawakili siku moja ya maisha yako na unaishi kuwa miaka 80; hizo ni punje 80 za mchanga. Kama ungeweza kushikilia punje 80 za mchanga mkononi mwako ingekuwa vigumu kutambua kama ni wewe? Pulizo kidogo inaweza kuiondoa mkononi mwako.

Kwa sababu ya mjadala, tuseme mrabaha inchi moja ya mchanga una mchanga 6000, au siku 6000. Ujazo mmoja wa kipimo cha mguu unawezaa kuwa na mchanga 10,368,000; huo ni mchanga mwingi kwa siku unaweza kuwa miaka 28405.

Unapoangalia punje zote za mchanga katika fuo zote za bahari (jumlisha mchanga wote ulipo kwenye inch kavu!) wa dunia, akili haiwezi kujua idadi ya siku au miaka.

Ikiwa kila punje ya mchanga unawakilisha siku, punje zote za mchanga wote ulimwenguni hauwezi kulingana na idadi ya wakati katika milele! Mbinguni au jehanamu.

Hupaswi kuacha milele kwa ajili ya furaha ya dhambi ya muda mfupi.

Ayubu 29: 18, "*Ndipo niliposema, nitakufa ndani ya kioto change, nami nitaziongeza siku zangu kama mchanga;*"

Hivyo ndio maana Ayubu aliweza kuvumilia kila kitu alichorushiwa na Shetani. Kiwango cha maisha ya mwanadaamu ni mchanga 70. Hiyo si kitu ukilinganisha na milele!

Starehe zote za maisha hayana thamani kulinganisha na milele jehanamu. Lakini, fikiria, ndugu na dada, kuhusu milele mbinguni. Hiyo itakuwa vizuri kiasi gani!

Wapendwa, nisikilizeni! Je unanisikia? Jehanamu ni usiku wa milele kwa kila mwenye dhambi anayeondoka ulimwenguni hapa bila Kristo! Wakati tunaoshi katika ulimwengu huu ni mdogo sana. Haiwezi kulinganishwa na milele.

Hakuna kutoka jehanamu

Kuna kutoka ulimwenguni hapa – kifo!

Kuna kutoka katika kuzimu – maana baada yake hukumu.

Lakini hakutakuwa na kutoka Jehanamu – mateso ya milele!

Kuna njia moja tu ya kuepuka jehanamu, na hiyo ni kutokwenda pale katika sehemu ya kwanza!

Milango ya jehanamu itafungwa milele. Kipindi cha mateso kwa waovu na wasiomcha Mungu itachukua muda mrefu kama ambavyo itakavyokuwa kwa mbingu kwa waliokolewa. Mat. 25:46, "*Na hao watakwendaa zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele.*"

Si afadhali utumie muda wako mbinguni?

Hakutakuwa na upumuaji

Siku ya hukumu itakuwa ni siku ya maangamizi kwa wenye dhambi na wasiomcha Mungu.

- 2 Pet. 3:7, "*Lakini mbingu za sasa na nchi zimewekwa akiba kwa moto, kwa neno lilo hilo, zikilindwa hata siku ya hukumu, nay a kuangamia kwao wanadaamu wasiomcha Mungu.*"
- 2 Thes. 1:7-9, "*Hata mkawa kielelezo kwa watu wote waaminio katika Makedonia, na katika Akaya. Maana kutoka kwenu neno la Mungu limevuma, si katika Makedonia na Akaya tu, ila na kila mahali imani yenu mliyo nayo kwa Mungu imeenea hata hatuna haja sisi kunena lolote. Kwa kuwa wao wenyewe wanatangazaa habari zetu, jinsi kulivyokuwa kuingia kwetu kwenu; na jinsi mlivyomgeukia Mungu mkaziacha sanamu, ili kumtumikia Mungu aliye hai, wa kweli.*"

Maangamizi katika siku hii ya kutisha haimanishi kupumua, lakini ni muendelezo; ni milele.

Hitimisho

Rafiki wapendwa, haipaswi kuwa hivyo.

Zaburi 23:1-6, "*BWANA ndiye mchungaji wangu, sitapungukiwa na kitu. Katika malisho ya majani mabichi hunilaza, kando ya maji ya utulivu huniongoza, katika njia ya haki kwa ajili ya jina lake. Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya; kwa kuwa wewe upo pamoja nami, gongo lako na fimbo yako vyaanifariji. Waandaa meza mbele yangu, machoni pa watesi wangu. Umenipaka mafuta kichwani pangu, na kikombe change kinafurika. Hakika wema na fadhili zitanifuata siku zote za maisha yangu; nami nitakaa nyumbani mwa BWANA milele.*"

Ulinganifu ulioje! Kifo kuingia mbinguni; au mlango wa kifo kuingia jehanamu!

Yesu mwenyewe alisema kwamba mwanadamu ana uchaguzi. Msikilize!

Marko 16:15-16, "*Akawambia enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka;asiyeamini atahukumiwa.*"

Maneno haya ya Kristo yalie mioyoni mwenu leo na katika siku zenu za maisha yenu:

Mat. 7:13-14, "*Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba; maana mlango ni mpana naa njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. Bali mlango ni mwembamba na njia imesonga iendayo uzimani nao waionao ni wachache.*"

Njia iendayo jehanamu ni njia pana ya Shetani – inaenda kuwa na watu wengi, lakini nafasi yako itakuwepo pia, kama ukisisitiza kwenda hapo.

Rafiki wapendwa, hakika uhitaji kwenda jehanamu!